## Maswali

1. Nani walikuja kupigana na Waisraeli?
2. Sauli alikuwa na watu wangapi kwa jeshi lake?
3. Yonathani alienda na nani kupigana na Wafilisti?
4. Yonathani aliuliza Mungu apeani ishara gani?
5. Wafilisti walipaza sauti kwa Yonathani eti nini?
6. Yonathani alienda namna gani ndiyo sababu aliwafikia Wafilisti bila kujua?
7. Mungu alituma nini kusaidia Yonathani?
8. Wafilisti walifanya nini?
9. Sauli na jeshi lake walifanya nini?
10. Nani aliokoa Waisraeli kutoka kwa Wafilisti?

## Majibu

1. Wafilisti walikuja kupigana na Israeli.
2. Sauli alikuwa na watu 600 pekee kwa jeshi lake.
3. Yonathani akaenda na mchukua silaha zake kupigana na Wafilisti.
4. Wafilisti wakisema, “Kuja penye tuko,” hapo Yonathani atajua kwamba Mungu atawasaidia.
5. Wafilisti walipaza sauti, “Kuja penye tuko.”
6. Yonathani alikwea kwa jabali ya mwamba akitambaa kwa miguu na mikono.
7. Mungu alituma mtetemko wa nchi kusaidia Yonathani.
8. Wafilisti waliogopa. Walitoroka, hali wanapigana wenyewe kwa wenyewe.
9. Sauli na jeshi lake walifukuza Wafilisti na wakashinda vita.
10. Mungu alisaidia Yonathani na mchukua silaha zake na akaokoa Waisraeli.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1    Mwaka wa 3**

# 25 Yonathani ni mjasiri

## Marejeo

1 Samweli 14: 1 – 23

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yonathani alikuwa na imani kwa Mungu tena aliamini kwamba ataokoa Waisraeli kutoka kwa madui wao.

## Maneno maalum

25.1 Sauli + mwana + Yonathani + amini Mungu + Wafilisti + jeshi kubwa + Sauli watu 600
25.2 Yonathani + mchukua silaha + Wafilisti + kuja penye tuko + Mungu anasaidia + mwinuko wa jabali ya mwamba
25.3 Yonathani + mchukua silaha + kwea jabali + Wafilisti + shangaa + Mungu anasaidia + mtetemeko wa nchi + toroka
25.4 Walinzi wa Sauli + Wafilisti + kutoroka + pigana wenyewe kwa wenyewe + Yonathani na mchukua silaha + Sauli na jeshi + shinda vita

**25.1** Sauli alikuwa mfalme kwa muda mrefu. Hakukuwa mfalme mzuri. Hakukuwa akifanya vile Mungu alitaka. Sauli alikuwa na mwana aliyeitwa Yonathani na alikuwa mjasiri, wa nguvu na mkarimu. Yonathani alimpenda Mungu tena alimwaamini.


Wafilisti walikuja kupigana na Israeli. Walipiga kambi yao juu ya kilima. Kila upande wa hicho kilima kulikuwa na jabali ya mwamba iliyoinuka sana. Ilikuwa vigumu kwa jeshi la Sauli kupanda juu na wawafikie. Wafilisti walikuwa na jeshi kubwa sana lakini Sauli alikuwa na watu 600 pekee. Watu wengi wa Sauli hawakuwa na panga wala mikuki. Hawakuwa na silaha za kupigania.

**25.2** Yonathani alikuwa kwa jeshi la Sauli. Siku moja aliambia kijana mchukua silaha zake, "Twenda kule tuonane na Wafilisti. Labda Mungu anaweza kuokoa watu wetu pamoja na nchi yetu. Anaweza kuokoa kwa urahisi na jeshi ndogo vile anaweza kuokoa na jeshi la watu wengi." Mchukua silaha wake alikubali kwenda na Yonathani.

Yonathani alisema, "Tutaenda tusimame penye Wafilisti wanaweza kutuona. Wakitwambia, 'Simama kule mpaka tuteremke penye mko, tutatulia pale.' Lakini wakisema, 'Kuja penye tuko,' tutaenda kule." Yonathani aliomba Mungu awasaidie. Aliomba kwamba Wafilisti wakisema, "Kuja penye tuko," atajua kwamba hiyo ni ishara kuonyesha Mungu atawasaidia washinde Wafilisti.

Yonathani na mchukua silaha zake walienda na kusimama penye Wafilisti wangeweza kuwaona. Wafilisti walianza kuwacheka na kuwafanyia msaha. Walisema, "Angalia, Waisraeli wako wanatoka kwa mashimo penye walikuwa wamejificha." Waliwapigia kelele na kusema, "Kuja mpaka penye tuko na tutamwonyesha kitu." Yonathani alijua Mungu ako nao. Yonathani alienda mbele na kufuatwa na mchukua silaha zake. Walipanda kwa huo mwinuko wa jabali ya mwamba wakitambaa kwa mikono na miguu. Hawakuogopa kwa sababu walijua Mungu atawasaidia.

**25.3** Wafilisti huko juu kwa jabali waliendelea kuwapigia kelele wakiwambia waende kule juu. Lakini hawakuamini kwamba wanaweza kupanda mpaka kule. Walijua ni vigumu mtu yeyote kupanda huo mwinuko wa jabali, kwa hivyo hawakuwa makini. Yonathani na mchukua silaha wake, walifika huko bila hao kujua. Hawakutarajia. Yonathani na mchukua silaha zake waliua Wafilisti ishirini kwa dakika chache sana.



Mungu aliwasaidia kwa kutuma mtetemko wa nchi. Kwa hivyo nchi ilitetemeka. Wafilisti waliogopa huo mtetemko. Tena wakaona watu wao wanauawa. Hawakujua kulikuwa na vijana wajasiri wawili tu waliokuwa wakiwashambulia. Walifikiri ni jeshi lote la Israeli lilikuwa linawashambulia. Nchi ilipoanza kutetemeka, waliogopa na kuanza kutoroka. Walitoroka hali wanapigana wenyewe kwa wenyewe.

**25.4** Mlinzi wa Sauli alienda kwa Sauli. Kuna mambo yasiyo ya kawaida yanaendelea kwa kambi ya Wafilisti. Wafilisti wanaonekana wanatoroka na wanapigana wenyewe kwa wenyewe. Sauli alijua kwamba lazima kuwe kuna mtu ameenda kwa kambi ya Wafilisti. Alihesabu watu wake na kupata kwamba Yonathani na mchukua silaha zake hawako.

Sauli alikusanya jeshi lake lote na kufuata Wafilisti. Sauli na jeshi lake walishinda vita na kufukuza Wafilisti kutoka kwa nchi yao. Kwa hivyo Waisraeli waliokolewa kutoka kwa maadui wao kwa nguvu za Mungu na ujasiri wa Yonathani na mchukua silaha wake.